

# »Kusimamisha maharagwe ya kutambaa«

Kujitengenezea vijiti husaidia kuzalisha maharagwe ya kutambaa.

Katika maeneo za nyanda ya juu, maharagwe ya kutambaa huzaa mara tatu kuliko maharagwe ya kichaka. Maharagwe ya kutambaa huhitaji vijiti ili yaza vizuri. Halfu, vizingi/vijiti bora huwa ghali.

## **Urefu bora wa vizingi/ vijiti**

Vizingi vinafaa kuwa na urefu wa mita mbili au mbili unusu. Vikiwa vifupi mno, ncha za maharagwe zitajikunja na kukatika kwa hivyo, mavuno hupunguka. Vizingi vikiwa virefu mno, maharagwe yatajitatihidi kutambaa kadri ya urefu huo na kuzaa kidogo. Maharagwe yanapokaribia wiki mbili au tatu, ncha za mimea huaza kutafuta sehemu za kujishikilia na kutambaa. Unafaa kuyawekea maharagwe vizingi wiki mbili baada ya kupanda. Laa sivyo, yatatambaliana kwenye udongo na kuzaa kidogo.

## **Vizingi vyatengenezea**

Ili kujitengenezea vizingi, panda miti mbao kama vile mikaratusi au mtukutu. Kata matawi ya miti ili kupata vizingi. Uwezekano wingine ni kutumia vizingi vyatengenezea nyasi ya napier. Shamba lako halifai kufunikwa na magugu ili maharagwe yasibaki chini yakinabaa juu ya magugu.

Weka vizingi katika mistari kila baada ya nusu mita na uache angalao nusu mita kati ya mistari. Simika vizingi kwa nguvu kwenye udongo ili visiangushwe na upemo mkali. Kila kigingi kinawezekana kusimamisha maharagwe matano. Ili kutengeneza henga, weka vizingi vitatu vyatengenezea urefu wa mita mbili kati ya mistari miwili ya maharagwe, kila kigingi kikiachana kwa mita 5.

Unganisha vizingi hivyo katika sehemu ya juu kwa kamba au fito.

Baada ya kuvuna, viweke vingi katika kivuli, ili visipasuliwe na juu. Simamisha vizingi ili pande iliokuwa ardhini iangalie juu, ili maji yatiririke na vikauke kwa urahisi.

Unapovuna mahindi, ondoa magunzi na majani kisha uacha mashina thabiti yakiwa yamesimama ili kuwa vizingi vya maharagwe msimu ujao. Ikiwa mashina ya mahindi si thabiti kutosha, unaweza kuweka vizingi vya miti katika kila mashina manne, na kuvifunga pamoja sehemu ya juu.

Unaweza pia kukuza maharagwe ya kutambaa pamoja na mahindi. Ili kuhakikisha kwamba maharagwe hayathiri mahindi, yapande mwezi mmoja baada ya mahindi.